

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Tarehe: 19/05/2020

TANGAZO LA ZABUNI
NAMBA LGA/166/2020/2021/NCS/1 Package 01-04
ZABUNI YA UKUSANYAJI USHURU MBALIMBALI WA VYANZO VYA MAPATO
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

Halmashauri ya Mji Makambako inakusudia kuweka Mawakala wa Utozaji Ushuru wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mwaka wa fedha **2020/2021.**

Halmashauri ya Mji Makambako inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo, watume maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

| NA. | AINA YA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO LA KUKUSANYA USHURU |
|-----|---|------------------------------------|--|
| 01. | Ukusanyaji wa ushuru wa mazao mengine ya chakula | LGA/166/2020/2021/NCS/1 package 01 | Eneo lote la Halmashauri ya Mji Makambako isipokuwa eneo la NFRA na soko la Nyanya |
| 02 | Ukusanyaji wa ushuru wa tozo ya choo soko kuu la Halmashauri ya Mji Makambako | LGA/166/2020/2021/NCS/1 package 02 | Eneo la soko kuu la Halmashauri ya Mji Makambako |
| 03 | Ukusanyaji wa ushuru wa zao la nyanya | LGA/166/2020/2021/NCS/1 package 03 | Eneo lote la Halmashauri ya Mji Makambako |
| 04 | kazi ya uzoaji wa taka ngumu kwa muda maalumu | LGA/166/2020/2021/NCS/1 package 04 | Eneo lote la Halmashauri ya Mji Makambako |

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Nyaraka za zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya kila zabuni husika. Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable). Mwombaji atalipa ada ya maombi ya **Tshs.100,000/= (laki moja tu)** Kwa kila zabuni, fedha zote zilipwe Ofisini kwa Mweka Hazina wa Halmashauri ya Mji Makambako.
2. Ombi la zabuni liwe na jina la zabuni anayoomba, aidha mwombaji aoneshe mahali ofisi yake ilipo.
3. Mwombaji atatakiwa kuambatanisha kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai, kivuli cha usajili wa kampuni, usajili wa **VAT/TIN** na **Nguvu ya kisheria “Power of Attorney”** miamala ya benki (bank statement) ya **miezi mitatu** kabla ya tarehe ya tangazo hili, pia aambatanishe wasifu wa kampuni **“Company Profile”** ya kampuni inayoomba kazi.

4. Mwombaji atatakiwa kutoza viwango halali vilivyoidhinishwa na sheria mama na sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mji Makambako.
5. Mwombaji aoneshe kiwango cha fedha atakacholipa kwa Halmashauri.
6. Iwapo mzabuni atachaguliwa, atatakiwa kuwasilisha dhamana ya utendaji "Performance guarantee" ya malipo ya **miezi miwili (2)** na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika na wanaotambulika, kabla ya kusaini mkataba
7. Mwombaji aambatanishe kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi.
8. Mwombaji aorodheshe vifaa alivyonyavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao. Pia mwombaji aoneshe uzoefu alionao katika zabuni hiyo.
9. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi, aina na namba ya zabuni anayoomba. Atatakiwa kutuma **kabrasha halisi (original) na nakala (copy) mbili (2)** yawekwe kwenye bahasha moja. Juu ya bahasha kusindikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya jina la zabuni, namba ya zabuni na anuani ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako.
10. Mwombaji atoe tamko la kutojijhusisha na vitendo vya rushwa.
11. Halmashauri haitalazimika kukubali zabuni ya chini au yoyote, uamuzi wa Bodi ya Zabuni juu ya uteuzi wa Mzabuni ni wa mwisho.
12. Maombi yafungwe kwenye **bahasha ya khaki yenye lakiri**. Juu ya bahasha ioneshwe aina ya zabuni na namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa anuani ifuatayo

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Mji Makambako,
S.L.P 405 Makambako**

Kabrasha la zabuni linapatikana katika ofisi za Halmashauri ya Mji Makambako, ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, kitengo cha Manunuzi. kuanzia siku ya Jumatatu hadi Ijumaa saa 1.30 Asubuhi hadi 9.30 Alasiri.

13. Maombi ya Zabuni zote yawasilishwe katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Makao Makuu Halmashauri ya Mji Makambako. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **01/06/2020 saa nne kamili(4) kamili Asubuhi**. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni utakaofanyika siku ya Jumatatu **tarehe 01/06/2020 saa sita (6) Mchana** katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.
14. Maombi yote yatakayochelewa kuwasilishwa baada ya **saa nne kamili(4)** Asubuhi hayatapokelewa.



Paulo S. Malala,
MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO